
SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

# TAARIFA YA MIAKA 50 YA MAADHIMISHO YA SHEREHE ZA MAPINDUZI YA ZANZIBAR



**TUDUMISHE AMANI, UMOJA NA MAENDELEO AMBAYO NI MATUNDA YA MAPINDUZI YETU, MAPINDUZI DAIMA**



**MHESHIMIWA ABEID AMANI KARUME**
**RAIS WA KWANZA WA ZANZIBAR**
**1964 - 1972**

**YALIYOMO** **UKURASA**


YALIYOMO .......... i
VIFUPISHO VYA MANENO .......... iii
DIBAJI .......... iv

SURA YA KWANZA .......... 1
HISTORIA FUPI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI .......... 1
1.1 Utangulizi .......... 1
1.2 Marais wa Zanzibar wa Awamu Mbalimbali Tokea Mwaka 1964 .......... 2
1.3 Mawaziri Walioiongoza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Kuanzia 1964 .......... 4
1.4 Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu .......... 6

SURA YA PILI .......... 10
MUUNDO WA ORMBLM ULIVYOBADILIKA KATIKA NYAKATI TOFAUTI KUANZIA MWAKA 1964 .......... 10
2.1 Utangulizi .......... 10
2.2 Muundo wa ORMBLM Awamu ya Kwanza (1964 - 1972) .......... 10
2.3 Muundo wa ORMBLM Awamu ya Pili (1972 - 1984) .......... 11
2.4 Muundo wa ORMBLM Awamu ya Tatu (1984 - 1985) .......... 12
2.5 Muundo wa ORMBLM Awamu ya Nne (1985 - 1990) .......... 12
2.6 Muundo wa ORMBLM Awamu ya Tano (1990 - 2000) .......... 13
2.7 Muundo wa ORMBLM Awamu ya Sita (2000 - 2010) .......... 14
2.8 Muundo wa ORMBLM Awamu ya Saba (2010 – 2013) .......... 15

SURA YA TATU .......... 17
MAJUKUMU NA MALENGO YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI .......... 17
3.1 Utangulizi .......... 17
3.2 Majukumu ya ORMBLM .......... 17
3.3 Malengo ya ORMBLM .......... 18

SURA YA NNE .......... 19
SERA NA SHERIA ZILIZOONGOZA ORMBLM .......... 19

4.1 Utangulizi ........................................................................ 19

SURA YA TANO ........................................................................ 21
MABADILIKO NA MATUKIO MAKUU KATIKA
MFUMO WA KISIASA, KIUTAWALA
NA KITEKNOLOJIA ........................................................................ 21
5.1 Utangulizi ........................................................................ 21
5.2 Mabadiliko ya Kisiasa ........................................................................ 21
5.3 Mabadiliko ya Kiteknolojia ........................................................................ 23
5.4 Mabadiliko ya Kiuchumi ........................................................................ 23
5.5 Mabadiliko ya kiutawala ........................................................................ 25

SURA YA SITA ........................................................................ 27
MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KUTOKA 1964 .................... 27
6.1 Utangulizi ........................................................................ 27
6.2 Sekta ya Sheria ........................................................................ 27
6.3 Rushwa na Uhujumu Uchumi ........................................................................ 27
6.4 Ziara za Ndani Zilizofanywa na Waheshimiwa
Marais wa Zanzibar ........................................................................ 28
6.5 Ziara za Nje za Waheshimiwa Marais wa Zanzibar ...................... 35
6.6 Ziara za Viongozi Walioitembelea Zanzibar ................................ 41
6.7 Mawasiliano na Viongozi, Watendaji wa Serikali na Wananchi...... 46
6.8 Mchango wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje .................... 48
6.9 Utawala Bora ........................................................................ 50
6.10 Kupunguza Umasikini ........................................................................ 51
6.11 Udhibiti na Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ............................ 51

SURA YA SABA ........................................................................ 53
CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA ........................................... 53
7.1 Utangulizi ........................................................................ 53

SURA YA NANE ........................................................................ 55
MATARAJIO YA ORMBLM PAMOJA NA TAASISI
ZAKE KATIKA MIAKA 50 IJAYO ........................................... 55
8.1 Utangulizi ........................................................................ 55

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | | |
|---|---|---|
| ASP | - | Afro - Shirazi Party |
| CD | - | Compact Disk |
| Dkt | - | Daktari |
| ERP | - | Economic Recovery Programme |
| DVD | - | Digital Video Disk |
| GSO | - | Government Security Office |
| INTOSAI | - | International Supreme Audit Institution |
| IT | - | Information Technology |
| MKUZA | - | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini |
| MTAKULA | - | Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula |
| Nd. | - | Ndugu |
| OKM | - | Ofisi kuu ya Kazi za Maendeleo |
| ORIUB | - | Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora |
| ORMBLM | - | Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi |
| SAP | - | Structural Adjustment Programme |
| SMZ | - | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| TANU | - | Tanganyika National Unity |
| TZS | - | Tanzania Shiling |
| UNDP | - | United Nation Development Programme Zanzibar |
| ZAFREZA | - | Zanzibar Free Port and Export Zone Authority |
| ZFPA | - | Zanzibar Free Port Authority |
| ZIPA | - | Zanzibar Investiment Programme Authority |
| ZPRP | - | Zanzibar Poverty Reduction Plan |

## DIBAJI

Tarehe 12 Januari mwaka 1964, Wananchi wa Visiwa vya Zanzibar walifanya Mapinduzi ya kuung'oa utawala wa Kisultani na kuweka Utawala na Mamlaka kwa Wananchi wa Zanzibar. Tukio hili limepelekea kila ifikapo tarehe 12 Januari ya kila mwaka, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wananchi kwa ujumla, kuadhimisha Mapinduzi hayo Matukufu.

Ifikapo Januari mwaka 2014, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa inatimiza miaka 50 tangu kufanyika Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeandaa kitabu hiki cha Maadhimisho ya Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa muongozo uliotolewa na Serikali. Kitabu hiki kimegawika katika sura nane ambazo zimebeba maudhui tofauti.

Sura ya Kwanza inaelezea historia ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ikijumuisha Marais walioshika nyadhifa katika awamu saba tofauti. Aidha, sura hii inaelezea na kuonesha picha za Mawaziri walioongoza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia mwaka 1964 pamoja na Makatibu Wakuu wa Baraza la Mapinduzi ambao pia kwa kipindi fulani walikuwa ndio Makatibu Wakuu wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Vile vile sura hii inaonesha Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu ambao waliiongoza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia mwaka 1995. Sura ya Pili inaelezea mabadiliko ya muundo wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika nyakati tofauti kuanzia mwaka 1964. Muundo huo, umekuwa ukibadilika kutokana na mahitaji ya Serikali na vipaumbele vya nchi. Mabadiliko hayo huwa yanahusisha kuongezeka au kupungua kwa Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii.

Sura ya Tatu inaelezea Majukumu na Malengo ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Majukumu hayo hubadilika kutokana na muundo uliopo wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na huwa unalenga kuongeza ufanisi wa Serikali katika kutoa huduma kwa wananchi.

Sura ya Nne inahusu Sera na Sheria zilizoongoza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tokea mwaka 1964. Baadhi ya Sheria hizo zimerithiwa kutoka katika Sheria za ukoloni na nyengine zimetungwa na vyombo vya kutunga Sheria vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, Sera mpya na Matamko mbalimbali ambayo yalitolewa na Viongozi wa Serikali kwa nyakati tofauti nayo yameainishwa katika sura hii.

Sura ya Tano imejikita katika kuonesha Mabadiliko na Matukio Makuu katika Mfumo wa Kisiasa, Kiutawala na Kiteknolojia. Mabadiliko hayo huwa ni chachu ya kuimarisha utendaji na maendeleo ya Ofisi na Serikali kiujumla ambayo huchangiwa zaidi na matukio yanayotokea Serikalini na kusababisha baadhi ya mfumo, shughuli au jukumu fulani ama kuongezwa au kupunguzwa kutegemeana na wakati na mahitaji husika. Sambamba na hilo, baadhi ya mabadiliko huchangiwa na mabadiliko ya mfumo wa Ulimwengu.

Sura ya Sita ya taarifa hii imeelezea mafanikio yaliyopatikana tokea mwaka 1964 katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mafanikio hayo yapo katika nyanja za kisheria, kijamii, kisiasa, kielimu, kiafya na kiuchumi. Sambamba na hayo, changamoto kadhaa zimejitokeza katika utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama zilivyoainishwa katika Sura ya saba. Aidha, sura ya nane ya taarifa hii imeonesha matarajio ya Ofisi kwa kipindi cha miaka 50 ijayo.

# SURA YA KWANZA

# HISTORIA FUPI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

## 1.1 Utangulizi

Kabla ya kufanyika kwa Mapinduzi Matukufu ya Januari 1964, Zanzibar ilikuwa ikiongozwa na Sheria za Kikoloni ambazo zilikuwa zikitungwa na Serikali ya Uingereza kupitia Baraza lake la Kutunga Sheria. Sheria hizo zililenga zaidi katika kuhakikisha Utawala wa Kikoloni pamoja na matakwa yao yanalindwa na kuimarika katika kipindi chote cha uongozi wao na kuwaacha Wananchi wa Zanzibar (Waafrika) kuwa ndio tabaka la chini lisilokuwa na haki wala utetezi wowote kupitia Sheria hizo.

Baada ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari, 1964, wananchi wa Zanzibar wakawa huru. Sheria zote zikawa zinatungwa na Baraza la Mapinduzi. Dikrii Namba 1 ya mwaka 1964 (The existing Laws Decree) ilitungwa na kuruhusu baadhi ya Sheria zilizokuwa zikitumika kipindi cha Ukoloni kuendelea kutumika kwa mujibu wa mazingira halisi ya Zanzibar na baadae Sheria nyengine za Kikoloni zilifutwa. Aidha, kupitia Sheria hizo, majengo kadhaa yalitaifishwa yakiwemo Jumba la Kasri la Sultani na kupewa jina rasmi la "Jumba la Wananchi" (People's Palace) na Jumba la Makaazi la Mwakilishi Mkaazi wa Uingereza likapewa jina rasmi la Ikulu ya Rais wa Zanzibar ambapo shughuli zote za Serikali zilifanyika.

Katika kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar, hatuna budi kujivunia kuwa na Serikali inayoongozwa na Rais anaechaguliwa na wananchi wenyewe. Rais wa Zanzibar ni alama ya uongozi na mtetezi wa Mapinduzi ya Zanzibar na mlinzi wa Katiba. Sheria zote za Serikali zilizopitishwa na Baraza la Mapinduzi na baadae Baraza la Wawakilishi la Zanzibar hutiwa saini na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kwa kawaida wananchi wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania husherehekea maadhimisho ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kila ifikapo tarehe 12 Januari, siku ambayo wananchi wa Zanzibar waliondokana na utawala wa kikoloni. Tarehe 12 Januari, 2014 ni miaka 50 sawa na nusu Karne tokea kufanyika kwa Mapinduzi ambapo sherehe hizi zinaadhimishwa kwa kauli mbiu ya: ***"Tudumishe Amani, Umoja na Maendeleo Ambayo ni Matunda ya Mapinduzi Yetu - Mapinduzi Daima".***

Lengo la Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwakomboa wanyonge wa Visiwa vya Unguja na Pemba kutoka mikononi mwa wakoloni na hatimae wananchi hao waweze kujitawala na kujiamulia mambo yao wenyewe katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ilitangaza dikrii tano za mwanzo ambazo zilikuwa muhimu katika kuanzisha mfumo wa Serikali. Dikrii Namba 4 ya tarehe 31 Januari, 1964 ambayo ilianza kazi mara baada ya Mapinduzi ilitoa muundo wa Baraza la Mapinduzi.

Kwa mujibu wa Dikrii hiyo, Rais wa Zanzibar alikuwa ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Kiongozi wa Nchi na Amiri Jeshi Mkuu. Aidha, chini yake kulikuwa na Makamo wa Rais ambaye alikuwa ni Msaidizi Mkuu wa Rais katika kutoa maamuzi ya kiutendaji.


## 1.2 Marais wa Zanzibar wa Awamu Mbalimbali Tokea Mwaka 1964

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tangu kuasisiwa kwake imeongozwa na Marais saba katika awamu tofauti.

Awamu ya kwanza ya Urais wa Zanzibar ilichukua miaka minane kuanzia mwaka 1964 hadi mwaka 1972, chini ya uongozi wa Muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Kiongozi wa pili kuingia Ikulu ni Mheshimiwa Mzee Aboud Jumbe Mwinyi aliyeshika uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzia mwaka 1972 hadi mwaka 1984. Awamu ya tatu ya uongozi ilianza mwaka 1984 hadi mwaka 1985 chini ya Mheshimiwa Mzee Ali Hassan Mwinyi. Uongozi wa Serikali ya awamu ya nne ulikuwa chini ya Marehemu Sheikh Idriss Abdulwakil kuanzia mwaka 1985 hadi mwaka 1990.

Mheshimiwa Dkt. Salmin Amour Juma aliongoza awamu ya tano ya Urais wa Zanzibar kuanzia mwaka 1990 hadi mwaka 2000. Kiongozi wa sita wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni Mheshimiwa Dkt. Amani Abeid Karume kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2010. Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni Rais wa awamu ya saba aliyeingia madarakani baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2010 na bado anaendelea wakati huu ambapo Zanzibar inaadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi.


## Picha za Waheshimiwa Marais Walioiongoza Zanzibar Tokea Kuasisiwa kwa Mapinduzi ya Zanzibar Mwaka 1964



MHESHIMIWA ABEID AMANI KARUME
RAIS WA KWANZA WA ZANZIBAR
1964 - 1972



MHESHIMIWA ABOUD JUMBE MWINYI
RAIS WA PILI WA ZANZIBAR
1972 - 1984



MHESHIMIWA ALI HASSAN MWINYI
RAIS WA TATU WA ZANZIBAR
1984 - 1985



MHESHIMIWA IDRISS ABDULWAKIL
RAIS WA NNE WA ZANZIBAR
1985 - 1990



MHESHIMIWA DKT. SALMIN AMOUR JUMA
RAIS WA TANO WA ZANZIBAR
1990 - 2000



MHESHIMIWA DKT. AMANI ABEID KARUME
RAIS WA SITA WA ZANZIBAR
2000 - 2010




MHESHIMIWA DKT. ALI MOHAMED SHEIN
RAIS WA SABA WA ZANZIBAR
2010 -

### 1.3 Mawaziri Walioiongoza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Kuanzia 1964

Mara tu baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964, Ofisi ya Rais ilikuwa inaongozwa na Waziri Mdogo Ofisi ya Rais Mheshimiwa Abdulaziz Ali Twala. Baadae mwaka huo huo, Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi ambapo shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zilikuwa zikisimamiwa na Ofisi hii.

Awamu ya pili ya uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzia mwaka 1972. Katika awamu hii, shughuli za Serikali zilikuwa zikiratibiwa kupitia Wizara ya Nchi chini ya Sekretarieti inayoongozwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi ambayo katika nyakati tofauti Viongozi mbalimbali wakiwemo Mawaziri na Makatibu Wakuu waliteuliwa kuongoza Wizara hiyo. Picha zifuatazo zinaonesha majina ya Mawaziri, Mawaziri Wadogo na Makatibu Wakuu walioiongoza Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Makatibu wa Baraza la Mapinduzi walioshika nyadhifa katika vipindi tofauti:


## Picha za Waheshimiwa Mawaziri Walioiongoza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Kuanzia Mwaka 1964



Mhe. Abdulaziz Ali
Khamis
1964 - 1967



Mhe. Aboud Jumbe
Mwinyi
1964 - 1972




Mhe. Hassan Nassor
Moyo
1972 - 1976



Mhe. Haji Khamis
Ussi
1977 - 1980



Mhe. Ali Mzee
Ali
1977 - 1980



Mhe. Ramadhan Haji
Faki
1980 - 1983



Mhe. Aboud Talib
Aboud
1980 - 1984




Mhe. Ali Hassan
Mwinyi
1983 - 1984




Mhe. Hafidh Suleiman
Almasi
1983 - 1984



Mhe. Ramadhan
Abdalla Shaban
1984 - 1985




Mhe. Ali Salim
Ahmed
1985 - 1988




Mhe. Taymour Saleh
Juma
1990 - 1995



Mhe. Iddi Pandu
Hassan
1989 - 1995



Mhe. Mohamed Ramia
Abdiwawa
1995 - 2000



Mhe. Suleiman Othman
Nyanga
2000 - 2003



Mhe. Dkt. Mwinyihaji
Makame
2003 -

### 1.4 Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu

Katika kipindi cha miaka 50 tokea kuasisiwa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964, ORMBLM iliongozwa na Makatibu Wakuu mbalimbali katika nyakati tofauti. Kuanzia mwaka 1964 hadi mwaka 1995, Katibu wa Baraza la Mapinduzi alikuwa pia ndie Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

**Picha za Makatibu Wakuu wa Baraza la Mapinduzi Ambao Pia Walikuwa Makatibu Wakuu wa ORMBLM Kuanzia Mwaka 1964 Hadi 1995**



Nd. Salim Said Rashid
Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
Januari 1964 - Aprili 1964



Nd. Rajab Saleh Salim
Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
Juni 1964 - Julai 1964



Nd. Ali Mohammed Omar
Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1964 – 1964



Nd. Makame Mzee Suleiman
Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
Octoba 1964 - Aprili 1972




Nd. Suleiman Ali Mnoga
Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1972 - 1976



Nd. Salmin Amour Juma
Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1976 – 1977



Nd. Ussi Khamis Haji
Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1977 – 1978



Nd. Ali Salim Mohamed
Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1978 – 1980



Nd. Mohamed Fakih Mohamed
Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1980 – 1981



Nd. Jaffar Mfaume Ali
Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1981 - 1984



Nd. Ahmed Abdulrahim Mahmoud
Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1985 – 1988



Nd. Mabrouk Jabu Makame
Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1988 - 1995

Aidha, Kuanzia mwaka 1995, vyeo hivi vilitofautishwa baina ya Katibu Mkuu Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

**Picha za Makatibu Wakuu Baraza la Mapinduzi Baada ya Kutofautishwa Vyeo Hivyo Kuanzia 1995 Hadi 2009**



Nd. Ahmed Mohamed Abdulrahman
Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1995 - 2003



Nd. Ramadhan Muombwa Mwinyi
Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
2003 - 2009

Katika mwaka 2010, cheo cha Katibu Mkuu Baraza la Mapinduzi kilibadilishwa na kuwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

**Picha ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi**



Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee
Katibu Baraza la Mapinduzi
na
Katibu Mkuu Kiongozi
2009 -

## Picha za Manaibu Makatibu wa Baraza la Mapinduzi



Nd. Thneyan Mohamed Suleiman
Naibu Katibu
Baraza la Mapinduzi
1964



Nd. Jaffar Khamis Burhan
Naibu Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1984 - 1985



Nd. Khamis Juma Chande
Naibu Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1985 - 1988



Nd. Yussuf Ali Salim
Naibu Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1989 - 2000



Nd. Ramadhan Muombwa Mwinyi
Naibu Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1995 - 2003



Nd. Makame Hussein Makame
Naibu Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1996 - 1998



Nd. Juma Bakari Juma
Naibu Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
1998 - 2000



Nd. Salum Maulid Salum
Naibu Katibu Mkuu
Baraza la Mapinduzi
2003 - 2010



Nd. Salmin Amour Abdalla
Naibu Katibu
Baraza la Mapinduzi
2010 -

**Picha za Makatibu Wakuu wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Kuanzia Mwaka 1995 Hadi 2013**



Nd. Mohamed A. Mohamed
Katibu Mkuu ORMBLM
1995 - 1999



Nd. Jaffar A. Juma
Katibu Mkuu ORMBLM
1999 - 2000



Nd. Mussa H. Mussa
Katibu Mkuu ORMBLM
2000 - 2010



Nd. Salum M. Salum
Katibu Mkuu ORIUB
2010 -

Aidha, Ofisi hii pia ilikuwa na Manaibu Makatibu Wakuu ambao baadhi yao wanaendelea hadi sasa.


**Picha za Manaibu Makatibu Wakuu wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**



Nd. Faharia Shomari
Naibu Katibu Mkuu
ORMBLM
1995 - 1998



Nd. Makame H. Makame
Naibu Katibu Mkuu
ORMBLM
1999 - 2000



Nd. Abdallah A. Abdallah
Naibu Katibu Mkuu Idara
Maalum za SMZ
2010 - 2012



Nd. Mwinyiussi H. Abdalla
Naibu Katibu Mkuu
TAMISEMI
2010 - 2013



Nd. Julius N. Maziku
Naibu Katibu Mkuu Idara
Maalum za SMZ
2012 - 2013



Nd. Said Abdalla S. Natepe
Naibu Katibu Mkuu
ORIUB
2010 -

# SURA YA PILI

# MUUNDO WA ORMBLM ULIVYOBADILIKA KATIKA NYAKATI TOFAUTI KUANZIA MWAKA 1964

## 2.1 Utangulizi

Muundo wa ORMBLM umekuwa ukibadilika mara kwa mara. Mabadiliko hayo yanatokana hasa ukizingatia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepitia katika awamu saba tofauti za uongozi na yalikuwa yanalenga kuongeza ufanisi, uwajibikaji na utendaji wa shughuli za Serikali. Katika kufanikisha azma hiyo, mabadiliko yaliyofanyika yalihusisha nafasi za uongozi na muundo wa ORMBLM. Sura hii inaonesha muundo wa ORMBLM namna unavyobadilika katika awamu tofauti.

## 2.2 Muundo wa ORMBLM Awamu ya Kwanza (1964 - 1972)

Mara baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964, hatua nyingi zilichukuliwa katika kuunda Serikali thabiti itakayokidhi haja ya wananchi wa Zanzibar. Aidha, katika awamu hii, Rais alikuwa ni Mwenyekiti wa Chama cha Afro-Shirazi Party (ASP) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Sura ya mwelekeo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu ya kwanza chini ya uongozi wa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, ilikuwa ni ya kishujaa kwani mazingira ya uwajibikaji yalihitaji ujasiri na ushujaa mkubwa. Azma kubwa ya kubeba taswira hiyo, ni kuweza kufanikisha lengo la kuweka misingi ya haki na usawa kwa watu wote wa Zanzibar.

Kutokana na hali hiyo, uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa awamu ya kwanza, mwelekeo wake ulikuwa ni kuleta ufumbuzi wa haki za wanyonge wa Zanzibar na kuwaletea heshima kama binaadamu wengine duniani. Uongozi wa awamu ya kwanza ulitekeleza kwa ufanisi mkubwa shabaha ya Mapinduzi kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Afro-Shirazi Party (ASP).

Katika awamu hii, ORMBLM ilikuwa ikiongozwa na Waziri Mdogo Ofisi ya Rais Mheshimiwa Abdulaziz Ali Khamis (Twala). Kwa upande wa Makatibu Wakuu, Ndugu Salim Said Rashid, Ndugu Rajab Saleh Salim, Ndugu Ali Mohammed Omar na Ndugu Makame Mzee Suleiman waliteuliwa kushika wadhifa huo katika vipindi tofauti. Baadae katika mwaka 1964, Mheshimiwa Mzee Abeid Amani Karume alifanya mabadiliko ya uongozi ambapo Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi alimteua kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais. Katika awamu hiyo, ORMBLM iliundwa na Taasisi na Ofisi zifuatazo:-

i. Afisi ya Huduma za Rais;
ii. Afisi ya Baraza la Mapinduzi;
iii. Idara ya Mipango na Uendeshaji;
iv. Idara ya Utumishi Serikalini;
v. Tume ya Utumishi; na
vi. Idara ya Usalama wa Taifa.

## 2.3 Muundo wa ORMBLM Awamu ya Pili (1972 - 1984)

Baada ya kifo cha Mzee Abeid Amani Karume mwaka 1972, Baraza la Mapinduzi lilimpendekeza kwa kauli moja, Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kikao cha Baraza la Mapinduzi kilichofanyika tarehe 10 Aprili 1972 na tarehe 11 Aprili 1972 Makao Makuu ya ASP Kisiwandui kilitoa azimio kwamba ***"Mzee Abeid Amani Karume ameuwawa na kuzikwa lakini kilichokufa na kuzikwa ni kiwiliwili chake tu, Chama na Baraza la Mapinduzi vipo pale pale. Mawazo, fikra, busara na maazimio yake yapo na yataendelea kudumishwa milele".*** Baada ya hapo safu mpya ya Uongozi iliundwa.

Katika awamu hii, ORMBLM iliongozwa na Mawaziri watano katika vipindi tofauti. Mawaziri hao ni Mheshimiwa Hassan Nassor Moyo, Mheshimiwa Haji Khamis Ussi Mlinde, Mheshimiwa Ali Mzee Ali, Mheshimiwa Ramadhan Haji Faki na Mheshimiwa Hafidh Suleiman Almasi. Aidha, katika kipindi hicho, Mheshimiwa Rais aliwateuwa Dkt. Salmin Amour Juma, Ndugu Suleiman Ali Mnoga, Ndugu Ussi Khamis Haji, Ndugu Ali Salim Ahmed na Ndugu Jaffar Mfaume Ali kuwa Makatibu Wakuu kwa nyakati tofauti. Katika kipindi hiki ORMBLM ilikuwa na muundo ufuatao:-

i. Afisi ya Huduma za Rais;
ii. Afisi ya Baraza la Mapinduzi;
iii. Idara ya Mipango na Uendeshaji;
iv. Idara ya Usalama;
v. Idara ya vyuo vya Mafunzo;
vi. Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo;
vii. Idara ya Kikosi Maalum cha Kujitolea;
viii. Jeshi la Kujenga Uchumi;
ix. Afisi ya Mwanasheria Mkuu;
x. Baraza la Wawakilishi;
xi. Idara ya Utumishi Serikalini;
xii. Tume ya Utumishi; na
xiii. Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale.

### 2.4 Muundo wa ORMBLM Awamu ya Tatu (1984 - 1985)

Awamu ya Tatu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianza rasmi mwezi Januari 1984, baada ya kujiuzulu Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi. Mheshimiwa Mzee Ali Hassan Mwinyi alichaguliwa kushika nafasi ya Urais wa Zanzibar, nafasi ambayo alidumu nayo kwa muda wa mwaka mmoja na nusu ambapo baadae alichaguliwa kushika nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika awamu hii, ORMBLM iliongozwa na Mheshimiwa Ramadhan Abdalla Shaaban ambapo Ndugu Jaffar Mfaume Ali na Ndugu Ahmed Abdulrahim Mahmoud waliteuliwa kuwa Makatibu Wakuu wa Ofisi hii kwa nyakati tofauti. Katika kipindi hiki, ORMBLM ilikuwa imeundwa na Ofisi na Idara zifuatazo:

i. Afisi ya Huduma za Rais;
ii. Afisi ya Baraza la Mapinduzi;
iii. Idara ya Mipango na Uendeshaji;
iv. Idara ya Utumishi Serikalini;
v. Tume ya Utumishi;
vi. Idara ya Usalama wa Siri za Serikali; na
vii. Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale.

### 2.5 Muundo wa ORMBLM Awamu ya Nne (1985 - 1990)

Kuchaguliwa kwa Mzee Ali Hassan Mwinyi kushika nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulitoa nafasi kwa Mzee Idriss Abdulwakil kushika nafasi ya Urais wa Zanzibar. Mheshimiwa Idriss Abdulwakil alipendekezwa na Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi, kugombea nafasi hiyo na baadae kushinda Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar uliofanyika mwezi Oktoba 1985.

Katika awamu hii, ORMBLM iliongozwa na Mheshimiwa Ali Salim Ahmed na Mheshimiwa Iddi Pandu Hassan ambao walikuwa Mawaziri wa Nchi Ofisi ya Rais kwa nyakati tofauti. Aidha, Ndugu Ahmed Abdulrahim Mahmoud na Ndugu Mabrouk Jabu Makame waliteuliwa kuwa Makatibu Wakuu wa Ofisi hii kwa nyakati tofauti. Aidha, Mheshimiwa Idriss Abdulwakil aliwateua Washauri wake watatu ambao ni; Dkt. Saleh Idrissa Mohamed (Kilimo), Khamis Hassan Ameir (Uchumi) na Ame Mohamed Juma (Mazingira Wilaya ya Mjini). Katika kipindi hiki ORMBLM ilikuwa imeundwa na Idara na Vitengo vifuatavyo:-

i. Idara ya Huduma za Rais;
ii. Idara ya Mipango na Uendeshaji;

iii. Idara ya Baraza la Mapinduzi;
iv. Tume ya Utumishi Serikalini;
v. Idara ya Utumishi Serikalini;
vi. Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale;
vii. Idara ya Usalama wa Siri za Serikali; na

**2.6 Muundo wa ORMBLM Awamu ya Tano (1990 - 2000)**

Awamu ya tano ilianza rasmi baada ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika Mwezi wa Oktoba 1990, ambapo Dkt. Salmin Amour Juma alichaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Awamu hii ilikuwa na mabadiliko makubwa katika safu za uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Dkt. Salmin aliendelea na mabadiliko katika safu za uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ambapo mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwezi wa Oktoba mwaka 1995, chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa, alimteuwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal kuwa Waziri Kiongozi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Katika mabadiliko hayo, Mheshimiwa Iddi Pandu Hassan na Mheshimiwa Balozi Mohammed Ramia waliteuliwa kuwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa nyakati tofauti wakati Ndugu Mohammed Ahmed Mohammed na Ndugu Jaffar Ali Juma waliteuliwa kuwa Makatibu Wakuu.

Sambamba na mabadiliko hayo, kwa mara ya kwanza Serikali ilianzisha nafasi ya Msemaji Mkuu wa Serikali ambapo Ndugu Hafidh Ali Tahir aliteuliwa kushika nafasi hiyo. Aidha, Mheshimiwa Dkt. Salmin Amour Juma alifanya uteuzi wa Washauri mbalimbali wakiwemo Mheshimiwa Mohammed Raza (Michezo), Mheshimiwa Bakari Abeid (Utamaduni), Mheshimiwa Haji Machano (Usalama), Mheshimiwa Mohamed Abbas (Vikosi vya SMZ), Mheshimiwa Simai Daima (Kilimo), Mheshimiwa Professa Saleh Idrissa (Kilimo), Waheshimiwa Said Iddi Bavuai, Said Rashid, Seif Rashid na Mohammed Mahmoud (Siasa). Aidha, Mheshimiwa Ali Mohammed Shoka (Mshauri wa Rais mambo ya Afya Pemba), Isaac Sepetu (Uhusiano wa Kimataifa). Katika kipindi hiki, ORMBLM iliendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli za Idara na Vitengo vifuatavyo:-

i. Idara ya Huduma za Rais;
ii. Afisi ya Baraza la Mapinduzi;
iii. Idara ya Mipango na Uendeshaji;
iv. Idara ya Mwanasheria Mkuu;
v. Idara ya Utumishi Serikalini;

vi. Idara ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
vii. Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo;
viii. Jeshi la Kujenga Uchumi;
ix. Idara ya Vyuo vya Mafunzo;
x. Kikosi cha Valantia;
xi. Tume ya Utumishi Serikalini;
xii. Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale;
xiii. Kitengo cha Mambo ya Uhusiano wa Kimataifa;
xiv. Ofisi ya Usalama wa Siri za Serikali;
xv. Kitengo cha Msemaji Mkuu wa Serikali; na
xvi. Idara ya Kazi Maalum.

### 2.7 Muundo wa ORMBLM Awamu ya Sita (2000 - 2010)

Awamu ya sita ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliongozwa na Mheshimiwa Dkt. Amani Abeid Karume baada ya kuchaguliwa na wananchi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000.

Mheshimiwa Rais aliteuwa Washauri ambao walimshauri katika masuala ya Siasa, Uchumi na Mazingira nao ni Mheshimiwa Ali Ameir Mohammed, Mheshimiwa Profesa Hamphrey P.B. Mushi na Mheshimiwa Abdalla Rashid. Aidha, Mheshimiwa Mbarak Salim Mbarak aliteuliwa kuwa Mshauri wa Rais mambo ya Mazingira - Pemba.

Katika awamu hii, ORMBLM ilikuwa inaongozwa na Mheshimiwa Suleiman Othman Nyanga na baadae Mheshimiwa Dkt. Mwinyihaji Makame wakati Ndugu Mussa Hassan Mussa alikuwa Katibu Mkuu. Katika Awamu hii Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale ilihamishiwa katika Wizara ya Elimu, Utamaduni na Michezo. Aidha, shughuli za Kitengo cha Msemaji Mkuu wa Serikali zilihamishiwa katika Idara ya Mawasiliano – Ikulu. Idara na Ofisi zilizounda ORMBLM ni hizi zifuatazo:-

i) Idara ya Huduma za Rais;
ii) Afisi ya Baraza la Mapinduzi;
iii) Idara ya Mipango na Sera;
iv) Idara ya Mawasiliano na Utoaji wa Habari– Ikulu;
v) Tume ya Utumishi Serikalini;
vi) Idara ya Utumishi Serikalini;
vii) Ofisi ya Usalama wa Serikali (GSO);
viii) Afisi ya Afisa Mdhamini – Pemba;
ix) Afisi ya Uratibu wa Uchumi na Uhusiano wa Kimataifa; na
x) Chuo cha Utawala wa Umma.

## 2.8 Muundo wa ORMBLM Awamu ya Saba (2010 – 2013)

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, awamu ya saba iliingia madarakani chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein ambapo uongozi wake unaendelea hadi hivi sasa wakati tunaadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein aliunda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa kwa mujibu wa maelekezo ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kama ilivyorekebishwa mwaka 2010.

Katika awamu hii, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein aliongeza majukumu kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Majukumu yaliyoongezwa ni ya Idara za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Idara Maalum za SMZ, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho ambazo hapo awali zilikuwa zikisimamiwa na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Aidha, Mheshimiwa Rais alianzisha Idara mpya ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi (Diaspora).

Katika hatua nyengine, kama ilivyokuwa katika awamu zilizopita Mheshimiwa Rais alifanya uteuzi wa Washauri watano wa Rais katika nyanja mbalimbali. Washauri hao ni; Mheshimiwa Balozi Mohammed Ramia Abdiwawa (Ushirikiano na Uwekezaji), Mheshimiwa Burhani Saadat Haji (Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi), Mheshimiwa Abrahman Mwinyijumbe (Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi), Mheshimiwa Issa Mohammed Issa (Mambo ya Utalii) na Mheshimiwa Sheha Mohammed Sheha (Mshauri wa Rais Pemba).

Katika muundo wa awali wa awamu ya saba, Tume ya Utumishi Serikalini, Idara ya Utumishi Serikalini na Chuo cha Utawala wa Umma zilihamishiwa katika iliyokuwa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha, muundo wa ORMBLM ulibadilika tena katika mwezi wa Agosti, 2013 na kuziondoa Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho na Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ. Katika mabadiliko hayo Idara ya Utawala Bora, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Idara ziliopo chini ya Tume ya Mipango zilihamishiwa katika Ofisi hii. Muundo mpya wa ORMBLM unajumuisha Ofisi na Idara zifuatazo:-

i) Ofisi ya Faragha;
ii) Ofisi ya Baraza la Mapinduzi;
iii) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;

iv) Idara ya Mawasiliano – Ikulu;
v) Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
vi) Ofisi ya Usalama wa Serikali (GSO);
vii) Ofisi ya Ofisa Mdhamini – Pemba;
viii) Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje;
ix) Idara ya Utawala Bora;
x) Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi;
xi) Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
xii) Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini;
xiii) Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi;
xiv) Idara ya Ukuzaji Uchumi; na
xv) Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

## SURA YA TATU

## MAJUKUMU NA MALENGO YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

### 3.1 Utangulizi

Majukumu na malengo ya ORMBLM huwa yanaainishwa kwa mujibu wa vipaumbele vya Serikali iliyopo madarakani katika kipindi husika. Kwa mantiki hiyo, majukumu na malengo hayo yamekuwa yakibadilika mara kwa mara kulingana na Mipango Mikuu ya Kitaifa, Sera za Kimataifa na kukua kwa Teknolojia. Mabadiliko ya majukumu yana lengo la kuongeza utoaji huduma na kustawisha ufanisi wa utendaji kazi.

Katika vipindi tofauti, viongozi walioiongoza ORMBLM wamekuwa wakisimamia utekelezaji wa majukumu mbalimbali. Miongoni mwa majukumu hayo ni pamoja na kushughulikia masuala ya fedha, mipango pamoja na mambo yanayohusu ushirikiano na uhusiano wa kikanda na kimataifa. Sura hii inaainisha majukumu na malengo ambayo utekelezaji wake unasimamiwa na ORMBLM.

### 3.2 Majukumu ya ORMBLM

Majukumu ya ORMBLM, ni pamoja na:-

i. Kusimamia shughuli za Mheshimiwa Rais na kujenga taswira nzuri mbele ya jamii;
ii. Kuendeleza na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mipango ya ORMBLM;
iii Kusimamia mambo yanayohusu Baraza la Mapinduzi
iv. Kuratibu Ushirikiano na uhusiano kikanda na kimataifa, pamoja na masuala ya Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi (Diaspora);
v. Kusimamia utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Usalama wa Serikali (GSO);
vi. Kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali, Wizara na Taasisi zake zote;
vii. Kuratibu misingi ya utawala bora ikiwemo maadili ya viongozi, kuzuia rushwa na haki za binaadamu;
viii. Kusimamia maendeleo ya uchumi wa Nchi; na
ix. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Dira 2020, MKUZA na Malengo ya Milenia.

### 3.3 Malengo ya ORMBLM

Malengo ya ORMBLM, ni pamoja na:-

i. Kuimarisha huduma za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
ii. Kuendeleza taswira nzuri ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
iii. Kuendelea kuandaa vikao vya kujadili Rasimu za Sera, Sheria na Nyaraka mbalimbali zinazowasilishwa katika vikao vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake;
iv. Kuimarisha uwezo wa watendaji katika Mipango, kuandaa na kuchambua Sera, kufanya Utafiti na shughuli za uratibu;
v. Kuongeza ufanisi wa kazi kwa kuimarisha mazingira ya utendaji kazi na maslahi ya wafanyakazi;
vi. Kuhakikisha kuwa Zanzibar inashiriki kikamilifu katika mikutano mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa;
vii. Kuwashajihisha Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii;
viii. Kuimarisha shughuli za upekuzi kwa watumishi kabla na baada ya kuajiriwa;
ix. Kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Kitaifa ikiwemo DIRA 2020, MKUZA II na Mkakati wa Kukuza Uchumi;
x. Kusimamia na kuratibu Mipango Bora ya watendakazi, Idadi ya watu pamoja na ustawi wa mama na mtoto kitaifa;
xi. Kuhakikisha kuwepo kwa Uchumi tulivu na madhubuti wenye kuhimili ushindani wa kimataifa unaolenga kuondosha Umaskini na kuinua ustawi wa hali za wananchi;
xii. Usimamizi wa uchumi na mipango ya maendeleo;
xiii. Kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali, Wizara na Taasisi zake zote;
xiv. Kuishirikisha Jamii katika kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi; na
xv. Kuimarisha Utawala Bora na Haki za Binaadamu kwa kuzingatia misingi ya Uwazi, Uwajiikaji na Ushirikishwaji.

# SURA YA NNE

## SERA NA SHERIA ZILIZOONGOZA ORMBLM

### 4.1 Utangulizi

Katika vipindi tofauti tangu kuasisiwa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Serikali imetoa matamko, Sera, mikakati na kutunga Sheria mbali mbali kwa ajili ya kuharakisha maendeleo ya wananchi wa Zanzibar yanafikiwa na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi. Miongoni mwa Matamko, Sera na Mikakati hiyo ni pamoja na:-

i. ***Mpango wa kufufua uchumi.*** Tamko hili lilikuwa na madhumuni ya kurekebisha hali mbaya ya uchumi iliyoikumba Zanzibar na hata Tanzania Bara kwenye miaka ya 1980;
ii. ***"Structural Adjustment Programme (SAP)"*** la mwaka 1982.
iii. ***Zanzibar ni Njema Atakae Aje.*** Tamko hili ni la mwaka 1984 ambalo lilikua linawataka Wazanzibari na wasio Wazanzibari kuja Zanzibar kuchangia katika harakati za kukuza uchumi na kuleta maendeleo;
iv. ***Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula (MTAKULA).*** Tamko hili ni la mwaka 1985 ambalo lilisaidia kuleta mapinduzi ya kilimo;
v. ***Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020***, Ilianzia mwaka 2000;
vi. ***Mpango wa Kupunguza Umasikini Zanzibar (ZPRP)***. Mpango wa mwaka 2002 hadi 2005;
vii. ***Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA I na MKUZA II).*** Mkakati wa mwaka 2005 na 2011;
viii. ***Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011;***
*ix. Mpango wa Mwelekeo wa Maendeleo ya Miaka 20 "20 Years Perspective Plan"; ulioanzia mwaka 1980 - 2000; na*
*x. Programu ya Mageuzi ya Kitaasisi na Maendeleo ya Watendakazi ya Mwaka 2010*

ORMBLM kwa nyakati tofauti, imeandaa miswada ya Sheria zinazosimamia utekelezaji wa majukumu ya Idara na Taasisi zilizo chini yake na kuiwasilisha katika Baraza la Wawakilishi kwa lengo la kuwa Sheria. Hatua hizi zimekuwa zikichukuliwa kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Taasisi na Idara husika. Aidha, zipo Sheria ambazo zilirithiwa kutoka Serikali ya Ukoloni zinazosimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi za Ofisi hii na zinaendelea kutumika. Sheria zifuatazo zinasimamia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii kuanzia mwaka 1964:-

i. Sheria ya Tume ya Uchunguzi Sura ya 33 ya mwaka 1922;
ii. Sheria ya Ofisi ya Usalama wa Serikali (GSO) Namba 5 ya mwaka 1983;
iii. Sheria ya Viapo na Uteuzi Namba 1 ya mwaka 1986;
iv. Sheria ya Mambo ya Rais Namba 5 ya mwaka 1993;
v. Sheria ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Namba 9 ya mwaka 2007;
vi. Sheria ya Tume ya Pamoja ya Rais Namba 10 ya 2001;
vii. Sheria ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Namba 11 ya mwaka 2003;
viii. Sheria ya Mamlaka ya Tume ya Haki za Binaadam na Utawala Bora kufanyakazi Zanzibar Namba 12 ya mwaka 2003;
ix. Sheria ya Muhuri na Bendera ya Rais Namba 10 ya mwaka 2004;
x. Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Namba 1 ya mwaka 2012;
xi. Sheria ya Kusimamia Mafao ya Viongozi Wastaafu wa Kisiasa Namba 2 ya mwaka 2012; na
xii. Sheria ya Tume ya Mipango Namba 3 ya mwaka 2012.

## SURA YA TANO

## MABADILIKO NA MATUKIO MAKUU KATIKA MFUMO WA KISIASA, KIUTAWALA NA KITEKNOLOJIA

### 5.1 Utangulizi

Katika hali ya kawaida, mabadiliko yanakusudia kuleta maendeleo kutoka hali duni kwenda katika hali bora iwe katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutawala au kisheria. Kwa tafsiri hiyo, ORMBLM nayo imepitia mabadiliko kadhaa tokea Mapinduzi Matukufu ya 1964. Mabadiliko hayo huwa ni chachu ya kuimarisha utendaji na maendeleo ya Ofisi na Serikali kiujumla.

Mabadiliko hayo huchangiwa zaidi na matukio ambayo hutokea Serikalini na kusababisha baadhi ya mfumo, shughuli au jukumu fulani ama kuongezwa au kupunguzwa katika Wizara kutegemeana na wakati na mahitaji husika. Sambamba na hilo, baadhi ya mabadiliko huchangiwa zaidi na mabadiliko ya mfumo wa Ulimwengu ambapo Zanzibar ni sehemu ya Ulimwengu huo. Hivyo, huwa haina budi kukabiliana au kwenda sambamba na mabadiliko yanayojitokeza.

Mabadiliko na matukio muhimu ambayo ORMBLM imeyatekeleza kwa vipindi tofauti yanaweza kugawanywa katika awamu mbalimbali za uongozi ambazo ORMBLM imezipitia ndani ya kipindi cha miaka 50 tokea Mapinduzi ya Mwaka 1964. Baadhi ya mabadiliko na matukio hayo ni haya yafuatayo:-

### 5.2 Mabadiliko ya Kisiasa

Mfumo na shughuli zote za utawala wa Wizara kuanzia miaka 1964 hadi 1984 zilikuwa zikiongozwa na Dikrii (Decree) ambazo baadhi ya Dikrii hizo zilirithiwa kutoka Ukoloni na nyengine zilikuwa zikitungwa au zikifanyiwa marekebisho siku hadi siku. Aidha, chombo kikuu kilichokuwa kinatumika kutunga Dikrii hizo kwa kipindi chote hicho ni Baraza la Mapinduzi.

Baada ya kuunganishwa kwa Chama cha ASP na TANU mwaka 1977, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais ambae hapo awali alikuwa ni Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango ya Chama cha ASP alipunguziwa jukumu hilo na kubakia kuwa ni Waziri wa ORMBLM.

Mabadiliko makubwa ya kisiasa katika awamu hii yalifanyika mwaka 1979 wakati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipotenganisha majukumu ya Mamlaka ya

kutunga Sheria na uendeshaji wa Serikali kwa kuanzisha Baraza la Wawakilishi ambayo hapo awali yalikuwa yakifanywa na Baraza la Mapinduzi. Chombo hicho kilisaidia sana kurahisisha utekelezaji wa majukumu na kuimarisha demokrasia hasa katika utungaji wa Sheria na usimamizi wa utendaji wa Serikali.

Katika mwaka 1984, Katiba mpya ya Zanzibar ilitungwa na kuifuta ile Katiba ya mwaka 1979 ambapo pamoja na mambo mengine iliimarisha zaidi demokrasia kwa kuainisha wazi haki za binadamu na mfumo mzima wa utawala pamoja na kutoa fursa kwa wananchi wa Zanzibar kuweza kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa kumchagua Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Wakati wa Utawala wa Chama kimoja, Idara Maalum za SMZ zilihusishwa moja kwa moja katika mfumo wa kisiasa ambapo kulikuwa na kamati za siasa ndani ya Idara hizo. Aidha, Idara hizo pia zilishiriki katika vikao mbalimbali vya Chama katika Mkoa wa Chama kijeshi huko Tanzania bara na Zanzibar. Baada ya kuanzishwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992, utaratibu wa Idara Maalum za SMZ wa kujihusisha na siasa ulifutwa kikatiba na kupelekea kila Idara Maalum kutoshiriki kabisa katika shughuli za kisiasa na kubakia na jukumu lake la msingi lililopangiwa na Sheria.

Sambamba na hilo, wakati wa uongozi wa Chama cha Afro-Shirazi kuliwekwa mtiririko wa ngazi za uongozi kuanzia eneo, Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Serikali ilitumia mtiririko huu wa ngazi za uongozi wa Chama kuweka viongozi wake. Makatibu wa Chama cha Afro-Shirazi wakawa pia ni Wakuu wa Wilaya na Mikoa. Ofisi zao ambazo ni sehemu moja wapo ya ngazi ya Chama zilikuwa pia ni sehemu ya Ofisi Kuu za Serikali katika Wilaya na Mikoa husika.

Ofisi hizi zilikuwa ni muhimu sana katika utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya Chama na Serikali vijijini. Katika mwaka 1992, Mabadiliko makubwa yalifanyika ambayo yalitenganisha nafasi za kisiasa kuwa tofauti na zile za kiutawala kwani Wakuu wa Wilaya na Mikoa walikuwa watendaji wa Serikali na sio wa kisiasa. Sambamba na hilo, marekebisho ya kumi ya Katiba ya mwaka 2010, yaliwaondoa Wakuu wa Mikoa kuwa ni miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kubakia na nafasi ya kiutendaji.

### 5.3 Mabadiliko ya Kiteknolojia

Mabadiliko ya Teknolojia kama zilivyo Ofisi nyengine za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na zile za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ORMBLM tokea mwaka 1964 hadi 1990 ilikuwa ikiendesha shughuli zake kwa kutumia teknolojia ya zamani. Kwa mfano, mfumo wa kutumia karatasi ndio uliokuwa ukitumika zaidi kutunza kumbukumbu za fedha na taarifa nyengine zote za Serikali kinyume na ilivyo sasa ambapo mbali ya utunzaji wa taarifa kwa njia ya karatasi, Compact Disk (CD), Digital Video Disk (DVD), Flash disk na Hard disk zinatumika kwa ajili ya kazi hiyo.

Kasi ya matumizi ya vifaa vya teknolojia ya kisasa ndani ya ORMBLM ilianza sambamba na matumizi ya teknolojia hiyo katika Bara la Afrika na baadhi ya Nchi nyengine duniani ikiwemo Urusi kwenye miaka ya tisini. Hatua hiyo ilipelekea ORMBLM kuanza kutumia Kompyuta za mezani (Desk Top Computers), mashine za kielektronik za kuchapia (Printers), Kompyuta ndogo za kuchukua mkononi (Laptop), Fotokopi, Skana, Nukushi na promptor kwa ajili ya kusomea ambazo sio tu zilirahisisha kazi, lakini pia ziliongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Katika mwaka 2007, kupitia msaada wa UNDP, Ofisi iliweka vifaa vya kisasa vya Mawasiliano ya Habari vikiwemo “Server” ambayo inatumika kwa kuwekea taarifa mbalimbali za Ofisi pamoja na kuweka waya za Mtandao wa ndani wa mawasiliano (local Area Network) ya Internet ulioziunganisha Ofisi zote za ndani. Aidha, mwaka 2011, Ofisi ilianzisha kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano sambamba na kuanzisha Tovuti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ijulikanayo kwa jina la www.ikuluzanzibar.go.tz pamoja na kutayarisha barua pepe rasmi za Maofisa wote na watendaji wengine.

### 5.4 Mabadiliko ya Kiuchumi

Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar umekuwa ukibadilika kutoka mwaka 1964 hadi hivi sasa chini ya usimamizi wa zilizokuwa Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango na Uchumi, Tume za Mipango, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na hatimae kwa sasa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Uchumi wa Zanzibar ulikuwa ukitegemea sana uzalishaji na biashara ya karafuu. Kutokana na ubora wa karafuu zake, Zanzibar iliweza kujihakikishia soko la kudumu na lenye bei nzuri kwa bidhaa hiyo duniani kote. Mauzo ya karafuu nje ya nchi yaliipatia Zanzibar wastani wa asilimia 90 ya pato ikiwa ni pamoja na fedha za kigeni kila mwaka.

Kutokana na hali hiyo kwa muda wa kipindi cha miaka minane ya Mapinduzi ya Zanzibar 1964 -1972 uchumi wa Zanzibar ulikuwa kwa kasi, hii ilitokana na kuongezeka kwa hakiba ya fedha za kigeni ambazo zilitokana na umaarufu wa kipekee wa Karafuu za Zanzibar katika soko la dunia ambapo imepelekea jumla ya tani 99,494.2 zenye thamani ya TZS. 1.2 bilioni kuuzwa nje ya nchi. Hali hii iliwezesha Serikali kusambaza huduma nyingi za kijamii kwa kipindi kifupi. Hadi kufikia miaka ya 1980, Uchumi wa Zanzibar ulikuwa umedhibitiwa na Serikali ambapo Serikali kuu ilibeba dhamana zote za utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na huduma nyingi za kijamii zilitolewa na kusimamiwa na Serikali, isipokuwa sekta ya kilimo ambayo kwa kiasi kikubwa ilikuwa chini ya sekta binafsi.

Hata hivyo, kushuka kwa uzalishaji wa zao la karafuu, sambamba na kushuka kwa bei ya bidhaa hiyo duniani katika miaka ya 80 kuliipelekea Zanzibar kuwa na haja ya kufanya mabadiliko makubwa ya mfumo wa uchumi wake.

Mwanzoni mwa miaka ya 1984, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliona umuhimu wa kuruhusu mfumo mzima wa kiuchumi kutoka mfumo wa uchumi uliodhibitiwa na Serikali kwenda katika mfumo wa uchumi huru na biashara huria. Hatua hii ilikwenda sambamba na kuanzishwa kwa Sera ya biashara huria pamoja na mabadiliko kadha ya Sera yakiwemo:-

i) Program ya Uimarishaji Uchumi ya Mwaka 1986 – 1988
ii) Sheria ya Uwekezaji Vitega Uchumi 1986
iii) Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha 1991
iv) Sheria ya Ukanda huru wa Kiuchumi 1992
v) Kuanzishwa kwa Bandari Huru 1998

Katika kipindi hicho cha 1980, mabadiliko na mageuzi mengi yalitokea ikiwa ni pamoja na kushushwa kwa thamani ya sarafu, kupanuliwa kwa huduma za uagizaji wa bidhaa, ili kuruhusu ushindani wa kibiashara na uchumi huru. Serikali iliendelea kutekeleza mageuzi ya kiuchumi kwa kuanzisha mpango wa 'Economic Recovery Programme' (ERP). Mpango huu ulikuwa na malengo ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kwa kutoa ruzuku kwa wazalishaji, kuimarisha miundo ya masoko, kuongeza rasilimali kwa ajili ya kilimo, kuzisaidia moja kwa moja shughuli za uzalishaji kwa kuifanyia matengenezo miundo mbinu iliyoharibika na kuongeza uwezo wa utumikaji wa viwanda.

Katika mwaka 1985 - 1986 palishuhudiwa ulazima wa kuandaa mikakati ya kushirikisha sekta binafsi katika kuongeza nguvu za kuimarisha uchumi na

kuchangia katika mfumo mpya wa kukuza uchumi. Sekta binafsi ilitakiwa kuchukuwa nafasi kubwa katika kukuza uchumi na kutafuta vyanzo mbadala. Utalii ulionekana kuwa ni kichecheo muhimu cha uchumi wa Zanzibar na sekta ya biashara ilifikia mchango wa wastani wa asilimia 19 katika mwaka 1986 hadi kufikia asilimia 30.2 mwaka 1994. Aidha, katika miaka ya 1985 hadi 1990 Serikali ililenga katika kuimarisha upatikanaji wa mahitaji ya msingi ya wananchi ikiwemo utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula (MTAKULA).

Katika kuimarisha uchumi, Taasisi mbali mbali ziliundwa katika kipindi hichi cha mabadiliko ya mfumo wa kiuchumi. Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), Mamlaka ya Maeneo Huru (ZAFREZA) na Mamlaka ya Bandari Huru Zanzibar (ZFPA) ni miongoni mwao. Taasisi hizi zilipewa majukumu ya kutangaza fursa za uwekezaji katika maeneo yaliyohusiana nayo kwa ajili ya kuvutia mitaji binafsi kuwekezwa nchini na kutimiza malengo ya Serikali yafuatayo:

i) Kukuza ajira kwa wazalendo.
ii) Kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi.
iii) Kukuza mapato ya Serikali kwa kuingiza utaalamu na teknolojia mpya nchini (transfer of skills/technology)
iv) Kuwapatia masoko wazalendo kwa bidhaa zinazoweza kutumika katika miradi ya uwekezaji (Backward/foward linkages to domestic economy)
v) Kutanua na kuimarisha wigo na uwiano wa kibiashara
vi) Kuongeza mapato katika fedha za kigeni

Malengo makuu ya kufanyika mabidiliko hayo ni kuimarisha uchumi imara na endelevu ambao utapelekea ukuaji mzuri wa uchumi, kasi ndogo ya mfumko wa bei, sarafu imara, na utoaji huduma wa gharama nafuu kwa wananchi.

**5.5 Mabadiliko ya kiutawala**

Zanzibar ni miongoni mwa nchi za awali kutunga Sheria madhubuti dhidi ya rushwa. Mnamo mwaka 1975 ilitungwa Sheria ya Kuzuia Rushwa iliyojulikana (Prevention of Corruption Decree Number 4 of 1975) na kuanzishwa Kamisheni mbili ili kusimamia Sheria hiyo. Kamisheni moja ilikuwa ikifanya kazi Unguja na nyengine Pemba. Mwaka 1985, Sheria hiyo ilifutwa na makosa yote yanayohusiana na rushwa yakaingizwa katika Sheria ya adhabu (Penal Act). Aidha, kikosi maalum kilianzishwa ndani ya Jeshi la Polisi kilichojulikana kwa jina la "Anti Corruption Squad" ambacho kilifanya kazi zinazohusiana na masuala ya kuzuia rushwa.

Aidha, mwaka 2004 Sheria ya Adhabu ilifutwa na kutungwa Sheria ya Makosa ya Jinai Namba 6 ya mwaka 2004 ambapo makosa yote yanayohusiana na rushwa yalijumuishwa katika Sheria hiyo.

Katika mwaka 2011, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipitisha Sera ya Utawala Bora ambayo ilipendekeza kuwepo kwa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi. Mwaka 2012, Sheria Namba 1 ya mwaka 2012 ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ilitungwa. Sheria hiyo ilipelekea kuanzishwa rasmi kwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar. Mamlaka hiyo imepewa majukumu ya kuchunguza makosa yote yanayohusiana na Rushwa na Uhujumu Uchumi, kuelimisha na kufanya tafiti mbali mbali ili kubaini mianya inayotumiwa na watu wasio waaminifu katika taasisi za umma na za binafsi katika kufanikisha vitendo vya rushwa au Uhujumu Uchumi. Katika utekelezaji wa jukumu hili Mamlaka hii ina wajibu wa kuzishauri taasisi hizo juu ya kushughulikia kasoro zilizoopo ili kuziba mianya hiyo. Aidha, Mamlaka ina jukumu la kutoa elimu ya uraia juu ya vitendo vya rushwa na Uhujumu Uchumi.

Katika hatua za kuimarisha Utawala Bora, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilichukuwa hatua kadhaa zilizolenga kuimarisha utawala bora nchini. Hatua hizo ni pamoja na kuundwa kwa Wizara ya Kuweka Hali za Wananchi Sawa ambayo ilikuwa na jukumu la kukuza ustawi wa wananchi. Aidha, kuanzishwa kwa Ofisi Kuu ya Maendeleo (OKM) kulikuwa na lengo la kusimamia masuala ya uongozi wa fedha. Katika mwaka 2000, kwa mara ya kwanza iliundwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba na Utawala Bora ambayo iliongozwa na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein na kupewa majukumu ya kusimamia masuala ya Utawala Bora.

Wizara hiyo ilikuwa na jukumu la kuratibu kwa mapana zaidi masuala ya Katiba, Utawala Bora, Sheria pamoja na kusimamia Taasisi za Kidini. Baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, shughuli zinazohusu Utawala Bora zilihamishiwa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora na baadae mwaka 2013 kuhamishiwa katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Katika eneo la Udhibiti na Ukaguzi wa Hesabu za Serikali, Zanzibar imekuwa ikitumia njia tofauti kuhakikisha kunakuwepo matumizi bora ya fedha na Mali za Umma kwa mujibu wa Sheria na viwango vya Kitaifa na Kimataifa vilivyowekwa na Jumuiya ya Taasisi za Ukaguzi Duniani (INTOSAI). Katika kukabiliana na mageuzi yanayoendelea Ulimwenguni kote, Serikali imetayarisha miongozo mbalimbali ya ukaguzi ikiwemo “Regularity Audit Manual”, “Performance Audit Guidelines”, “Information Technology Audit Guidelines” na “Environment Audit Guidelines”.

# SURA YA SITA

## MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KUTOKA 1964

### 6.1 Utangulizi

Katika kipindi hiki ORMBLM imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kupitia Idara na Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Ofisi hii. Majukumu ya ORMBLM yaliongezeka kulingana na muundo mpya wa Serikali ambapo hivi sasa Ofisi hii imekuwa ikisimamia na kuratibu utekelezaji wa Taasisi na Idara 15. Kipindi cha miaka 50 tokea baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Ofisi hii imepata mafanikio makubwa ya kupigiwa mfano. Mafanikio hayo yametokana na juhudi za makusudi zilizochukuliwa na wasimamizi wa majukumu mbalimbali ya ORMBLM, ambapo mafanikio hayo yanalenga kuleta uwajibikaji katika Ofisi na kuharakisha hatua za maendeleo ya Zanzibar na wananchi.

### 6.2 Sekta ya Sheria

ORMBLM imefanikiwa kuandaa Sheria zisizopungua 75 ambazo zinatumika kuongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sheria zote hizo zilitungwa na Baraza la Mapinduzi kuanzia mwaka 1964 hadi 1979. Aidha, Sheria 12 zimetungwa baada ya kuundwa kwa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar mwaka 1984 ambazo zinatumika kuongoza ORMBLM kwa lengo la kusimamia utendaji na kuweka muongozo wa kisheria.

Sambamba na hilo, ORMBLM imefanikiwa kuandaa Sera na kusimamia matamko ambayo huwa yanatolewa na Marais walioiongoza Zanzibar kwa kipindi chote cha miaka 50. Aidha, Ofisi imefanikisha kuandaa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020 (Vision 2020). Dira hii ndio muongozo mkuu wa muelekeo wa Sera, Sheria, Mipango na Mikakati yote ya kiuchumi, kisiasa na Kijamii Zanzibar. Hivyo Sera, Sheria, Mipango na Mikakati mbalimbali ya muda mfupi, kati na mrefu imeandaliwa kuendana na malengo na matarajio ya Dira hii. Sera hizo huongeza ari na utendaji katika ngazi zote za Serikali kwa watendaji pamoja na wananchi kupata mwelekeo na miongozo ambayo hutumika ili kufikia malengo ya kimaendeleo yaliyokusudiwa.

### 6.3 Rushwa na Uhujumu Uchumi

Mapambano dhidi ya Rushwa ni jambo muhimu sana kwa maendeleo ya Nchi yetu kama ilivyoelezwa katika mipango mikuu ya kitaifa ikiwemo Dira 2020 na MKUZA I na II unatambua kwamba vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi

sio tu vinapelekea kuwepo kwa uchumi, siasa na jamii duni lakini pia ni chanzo cha kuwepo umasikini uliokithiri. Kwa kutambua hilo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeanzisha chombo maalum kilichopewa jukumu la kudhibiti mianya ya Rushwa na Uhujumu Uchumi.




*Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora Dkt. Mwinyihaji Makame (wa tatu kutoka kushoto waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi mbalimbali baada ya kufunga mafunzo ya awali ya Uchunguzi kwa watumishi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar huko Kama Septemba 28, 2013*

### 6.4 Ziara za Ndani Zilizofanywa na Waheshimiwa Marais wa Zanzibar

Baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Mwaka 1964, Marais wa Zanzibar wamekuwa na utamaduni wa kufanya ziara ndani ya Visiwa vya Zanzibar kwa nyakati tofauti ambapo ORMBLM huratibu ziara hizo kwa ufanisi mkubwa. Katika ziara za ndani, Waheshimiwa Marais hutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo na kupata fursa ya kuzungumza na wananchi pamoja na watendaji wa Mikoa na Wilaya.

Matokeo ya ziara hizo, huwa ni kuimarika kwa utendaji katika Mikoa na Wilaya na kuimarika huduma za jamii. Aidha, wananchi hupata fursa ya kuonana na Viongozi wao na kubadilishana mawazo, fikra na ushauri sambamba na kupatiwa ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazokabili utekelezaji wa majukumu katika

ngazi hizo. Picha zifuatazo zinaonesha ziara za Marais wa Zanzibar wa awamu tofauti katika ngazi za Mikoa na Wilaya:-



*Rais wa awamu ya kwanza wa Zanzibar Mheshimiwa Mzee Abeid Amani Karume, akiangalia ramani ya njia mpya itokayo Bumbwini hadi Mahonda alipofika Bumbwini Misufini mwezi wa Novemba 1965.*



*Rais wa awamu ya pili wa Zanzibar Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi, akikagua ujenzi wa Hoteli ya Kitalii ya Bwawani iliyopo Malindi Funguni mwezi wa Mei 1973.*



*Rais wa awamu ya tatu wa Zanzibar Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, akipokea zawadi ya gunia la viazi kutoka kwa Wananchi wa Tawi la Makangale Pemba mwezi wa Disemba 1984.*



*Rais wa awamu ya nne wa Zanzibar Mheshimiwa Idriss Abdulwakil, akiangalia miche ya minazi katika Shamba la Serikali Selem Zanzibar alipotembelea shamba hilo mwaka 1986.*



*Rais wa awamu ya tano wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Salmin Amour Juma, alipowatembelea majeruhi katika hospitali ya Mnazi Mmoja waliopata ajali huko Mdodopilau Mkoa wa Kaskazini Unguja walipokuwa wakikimbiza mwenge Oktoba 8, 1996.*



*Rais wa awamu ya sita wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Amani Abeid Karume, akikata utepe kufungua madarasa mpya ya kusomea Skuli ya Ungi Msuka Pemba, alipokuwa katika ziara kuangalia maendeleo ya Elimu Disemba 14, 2009.*



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akipita juu ya tuta la kuzuia maji ya chumvi lililojengwa na Wizara ya Kilimo na Mali Asili katika kuhakikisha kuwa wananchi wanaondokana na usumbufu katika kilimo cha Mpunga wanaoupata katika Bonde la Ukele Mziwanda Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba Aprili 16, 2012*



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akifungua mradi wa maji safi na salama uliojengwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Wananchi wa Jimbo la Ziwani, Serikali ya Japan na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa huko Ziwani Mkoa wa Kusini Pemba April 20, 2012.*



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akipata maelezo wakati alipokuwa akitembelea shamba la migomba la ushirika huko Makunduchi Wilaya ya Kusini Unguja Mei 08, 2012.*



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akiangalia maonesho ya kazi za vikundi vya wajasiriamali vya Nungwi Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja Machi 2013.*



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Rans Co. Ltd, Ndugu Nassor Salim Said alipotembelea Kilimo cha mboga mboga kinacholimwa na Kampuni hiyo huko Kombeni Wilaya ya Magharibi, Mkoa wa Mjini Magharibi Machi 6, 2013.*



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Viongozi pamoja na Watendaji wa Mkoa wa Kusini Pemba wakati wa majumuisho ya ziara yake aliyoifanya Mkoani humo Machi 2013.*

**6.5 Ziara za Nje za Waheshimiwa Marais wa Zanzibar**

Katika kukuza ushirikiano wa kimataifa, miongoni mwa nchi marafiki za mwanzo kuyatambua Mapinduzi ya Zanzibar ni China, Cuba, Ujerumani Mashariki, Misri na Urusi. Nchi hizi zimekuwa mstari wa mbele katika kusaidia juhudi za maendeleo ya Zanzibar. Katika kipindi cha miaka 50, Zanzibar imepata mafanikio makubwa ya kuimarisha mahusiano na nchi mbalimbali ambapo Viongozi wa Nchi walipata fursa ya kutembelea na kujifunza juu ya namna ambavyo Nchi hizo zimepiga hatua katika kujiletea maendeleo yao.

Zanzibar imefaidika sana na ziara za nje ambazo hufanywa na Marais. Kwa mfano, katika ziara iliyofanywa na Rais wa kwanza wa Zanzibar Nchini Misri mwaka 1968 iliimarisha uhusiano na udugu baina ya Nchi zetu mbili uhusiano ambao umedumu hadi leo. Aidha, ziara zilizofanywa katika Nchi ya Libya ziliiwezesha Zanzibar kupata msaada mkubwa wa lami ambao uliimarisha miundombinu ya barabara Mijini na Vijijini.

Katika ziara ya hivi karibuni Nchini Vietnam, Zanzibar ilijifunza namna ambavyo nchi hiyo imepiga hatua kubwa ya kujiletea maendeleo katika muda mfupi ikiwemo kuzalisha mpunga kwa wingi. Vile vile, Zanzibar ilifaidika kwa

kuona na kufikia maelewano ya kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maendeleo Vijijini ya Vietnam. Maeneo mengine ambayo Vietnam ilikubali kushirikiana na Zanzibar ni katika Sekta ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambapo wananchi watashajihishwa kufuga samaki na mazao ya baharini kupitia vikundi vya ushirika pamoja na kunyanyua shughuli za akinamama wajasiriamali.

Katika ziara ya Jamhuri ya Watu wa China, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein alipata fursa ya kukutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Jamhuri ya Watu wa China Mheshimiwa Xi Jinping. Katika mazungumzo yao, Viongozi hao walikubaliana kukuza ushirikiano katika nyanja za kiuchumi na kijamii zikiwemo sekta za kilimo, uvuvi, afya, mafunzo mbalimbali, utafiti na utalii. Zifuatazo ni baadhi ya picha za Waheshimiwa Marais katika ziara zao Nchi za Nje:-




*Rais wa awamu ya tatu wa Zanzibar Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, akiteremka katika ndege wakati alipoitembelea Pyongyang (Korea) Aprili 9, 1985*



*Rais wa awamu ya nne wa Zanzibar Mheshimiwa Idriss Abdulwakil akisalimiana na Meya wa Jiji la Shanton nchini China Bwana Chen Yanfa, wakati alipoitembelea nchi hiyo mwezi wa Juni, 1990*



*Rais wa awamu ya tano wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Salmin Amour Juma, alipotembelea Nchi ya Iran na kuonana na Viongozi wa Nchi hiyo mwezi wa Oktoba, 1999.*




*Rais wa awamu ya sita wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Amani Abeid Karume, (wa pili kulia) aliposhiriki katika Mkutano wa uwekezaji, katika ukumbi wa The Greth Hall Nchini Uingereza Machi 10, 2009.*




*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein na Rais wa Uturuki Mheshimiwa Abdullah Gul wakifuatana baada ya mazungumzo ya pamoja yaliyofanyika Ikulu ya Rais Gul Nchini Uturuki wakati Mheshimiwa Dkt. Shein na Ujumbe wake walipokuwa katika ziara ya Kiserikali nchini humo April 29, 2011.*



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, alipokutana na Mfalme wa Ras Al Khaimah Sheikh Saud bin Sagr Al Qassimi, katika makaazi yake alipokuwa katika ziara ya Ras Al Khaimah, UAE Mwezi wa Julai, 2012.*



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akisalimiana na Rais wa Vietnam Mheshimiwa Truong Tan Sang, alipofika Ikulu ya Nchi hiyo katika ziara rasmi ya Kiserikali nchini humo  Novemba 23, 2012.*



*Rais wa awamu ya saba Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, (katikati kushoto) akiwa na ujumbe wake katika mazungumzo na Uongozi wa Serikali ya Jumhuri ya Watu wa China ukiongozwa na Rais wa Nchi hiyo Mheshimiwa Xi Jinping, (katikati kulia) wakati alipofanya ziara ya Kiserikali Nchini humo Mei 28, 2013.*



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akisalimiana na Waziri Mkuu wa Serikali ya Uholanzi Mheshimiwa Mark Rutte, alipofika katika Ofisi ya Waziri Mkuu huyo The Hegue Nchini Uholanzi  Agosti 28, 2013.*

## 6.6 Ziara za Viongozi Walioitembelea Zanzibar.

Katika kudumisha uhusiano na nchi nyengine, Zanzibar iliendelea kutembelewa na wageni mbalimbali katika ngazi ya Wakuu wa Nchi na Serikali, Mawaziri, Mabalozi na Viongozi wengeine wa Kimataifa. Katika diplomasia, kutembelewa na wageni ni hatua muhimu ya kukuza uhusiano na pia ni kielelezo cha Sera ya Nchi kukubalika na Mataifa mengine na Mashirika ya Kimataifa. Baadhi ya wageni mashuhuri walioitembelea Zanzibar katika kipindi cha miaka 50 wanaonekana katika picha zifuatazo:-



*Rais wa awamu ya kwanza wa Zanzibar Mheshimiwa Mzee Abeid Amani Karume, akimpokea Rais wa Shirikisho za Jamhuri ya Yugoslavia, Bwana Josip Bros Tito wakati alipoitembelea Zanzibar Januari 30, 1970*



*Rais wa awamu ya pili wa Zanzibar Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi, akimkaribisha mgeni wake Queen Elizabeth alipotembelea Zanzibar mwaka 1979.*



*Rais wa awamu ya nne wa Zanzibar Mheshimiwa Idriss Abdulwakil, akisalimiana na mgeni wake Balozi wa India Nchini Tanzania Bwana Hardev Bhalla alipomtembelea Ikulu Zanzibar mwezi wa Oktoba 1986.*



*Rais wa awamu ya tano wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Salmin Amour Juma, akimkaribisha Mgeni wake Rais wa Malawi Mheshimiwa Kamuzu Banda Mwezi wa Oktoba, 1991.*



*Rais wa awamu ya sita wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Amani Abeid Karume, akiwa na Rais wa DRC Mheshimiwa Joseph Kabila alipotembelea Zanzibar mwaka 2001.*



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akizungumza na mgeni wake Mtoto wa Malkia wa Uingereza Prince Charles, mara baada ya kuwasili Ikulu Mjini Zanzibar, akifuatana na Mkewe Camilla, Duchess of Cornwall Novemba 8, 2011.*



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akisalimiana na Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Watu wa China Hui Liangyu alipofika Ikulu Mjini Zanzibar Septemba 6, 2012.*



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Rais wa Jamhuri ya Watu wa China Xi Jinping katika hoteli ya Serena, Dar es Salaam alipotembelea Tanzania mwezi wa Machi, 2013.*



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akiwa katika mazungumzo na Rais wa Marekani Mheshimiwa Barack Obama Ikulu ya Dar es Salaam alipotembelea Tanzania mwezi wa Julai, 2013.*



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akisalimiana na Rais mstaafu wa Marekani Mheshimiwa Bill Clinton alipotembelea Ikulu Zanzibar mwezi wa Agosti, 2013.*

## 6.7 Mawasiliano na Viongozi, Watendaji wa Serikali na Wananchi

Moja kati ya mafanikio ya kujivunia katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ni hatua ya kuimarisha mawasiliano kati ya watendaji wa Serikali na wananchi kwa kupitia utaratibu maalum aliouanzisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein amekuwa akikutana na watendaji wote wa Serikali kila baada ya muda maalum kuzungumzia utekelezaji wa mipango ya kazi za Taasisi sambamba na utekelezaji wa bajeti. Picha inayofuata inamuonesha Mheshimiwa Rais akiwa katika moja ya mikutano ya Viongozi na Watendaji wa Serikali:-



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein akiwa katika mkutano wa Viongozi na Watendaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mwezi wa Aprili, 2013.*

Kuundwa kwa Idara ya Mawasiliano Ikulu kumeimarisha taswira nzuri ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa wananchi. Katika kutekeleza majukumu yake, Idara huandaa mikutano na waandishi wa habari ikiwa ni mpango mwengine wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar wa kuhakikisha kuwa wananchi wanaarifiwa ipasavyo kuhusu utekelezaji wa Sera na Mipango ya Maendeleo. Uamuzi wa kununua gari maalum kwa ajili ya matangazo ulikuwa na lengo hilo hilo la kuimarisha mawasiliano.



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein akiwa katika picha ya pamoja na Waandishi wa Habari waliofika Ikulu Zanzibar kwa ajili ya Mkutano mwezi wa Novemba 2011.*

**6.8 Mchango wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikifanya juhudi za makusudi za kuongeza pato la Nchi kwa kutumia mbinu mbalimbali. Katika kufanikisha hilo, Serikali imeweka mazingira mazuri ya kuwahamasisha Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kutoa michango yao ambayo inasaidia kuimarisha sekta mbali mbali zikiwemo za Afya na Elimu Unguja na Pemba. Juhudi hizo zimeanza kuzaa matunda ambapo maeneo kadhaa ya kijamii yameanza kufaidika na misaada yao. Baadhi ya Skuli zilizonufaika na misaada hiyo ni pamoja na:-

(a) Skuli ya Miti Ulaya – Wete imepokea msaada wa Kompyuta sita kutoka kwa Jumuiya ya Wazanzibari wanaoishi Uingereza.

(b) Skuli ya Kwale – Gombani ya Kale imepokea msaada wa meza 113, viti 252, meza kubwa 5 na viti 30 vya Ofisi ya Walimu kutoka kwa Wazanzibari wanaoishi Denmark.

(c) Skuli ya Ziwani imepokea msaada wa meza 149, viti 242, vyarahani 25 kwa ajili ya mradi wa Skuli, Kompyuta 103 kutoka kwa Wazanzibari wanaoishi Denmark.

(d) Skuli ya msingi ya Unguja Ukuu imefanyiwa matengenezo makubwa na Wazanzibari wanaoishi nchini Canada. Matengenezo hayo yamehusisha ujenzi wa madarasa 13, Ofisi tatu, stoo moja na chumba cha kompyuta.



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akipata maelezo wakati alipotembelea madarasa ya kusomea wanafunzi katika Skuli ya Unguja Ukuu yaliyofanyiwa matengenezo na Umoja wa Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi (Diaspora) Mei 7, 2012.*

Kwa upande wa sekta ya afya, Wazanzibari wanaoishi nchini Canada wamechangia mambo yafuatayo:-

(a) Vifaa vya matibabu ya meno katika Hospitali ya Cottage ya Makunduchi pamoja na kutoa huduma ya matibabu ya meno kupitia "Outreach Program" katika maeneo ya Matemwe. Aidha, hospitali ya wagonjwa wa afya ya akili Kidongo Chekundu imenufaika na msaada wa madawa.

(b) Msaada wa vitanda, kiti cha kung'olea meno, viti vya kukalia na vifaa vyengine vyenye thamani ya TZS. 50 milioni umetolewa na Wazanzibari wanaoishi Uingereza katika hospitali ya Jimbo la Kwamtipura.

(c) Msaada wa vitanda 4, meza 4, vifaa vya kuwekea "Drips" pamoja na mashine 6 za kuchunguza mapigo ya moyo (Cardiac Monitors) umetolewa katika Hospitali ya Chake Chake.



*Rais wa awamu ya saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akipata maelezo kutoka kwa Daktari wa Hospitali ya Makunduchi kuhusu Mashine ya Matibabu ya meno iliyotolewa na Wazanzibari Wanaoishi Nchini Canada Mei 24, 2011.*

Kupitia mpango wa majaribio wa kutuma fedha kwa kutumia mtandao wa wakala wa 'World Remit' unaotekelezwa na Benki ya Watu wa Zanzibar kuanzia tarehe 8 Februari 2013 hadi kufikia tarehe 31 Julai 2013 jumla ya miamala 620 yenye thamani ya TZS. 267,969,572 ilifanyika. Takwimu kutoka Benki Kuu ya Tanzania zinaonesha kwamba katika mwaka 2012, kwa wastani, Wazanzibari wanaoishi na kufanya kazi nchi za nje wameingiza fedha nchini (remittance) zenye thamani ya dola za Kimarekani 729,643.04 sawa na TZS. 1,182,021,724.8/= kwa mwezi. Fedha hizi zinatoka nchi tofauti, zikiwemo Canada, Sweden, Uingereza, Ujerumani, Norway, Australia, Finland, Ireland, Uholanzi, Denmark, Belgium, Zambia na Ufaransa.

### 6.9 Utawala Bora

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeimarisha Utawala Bora kwa kuchukua hatua mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya Kitaifa na Kimataifa. Miongoni mwa hatua ambazo zimechukuliwa ni kupitisha Sera ya Utawala Bora ambayo imeweka misingi na vipimo vya Utawala Bora Zanzibar. Aidha, Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Zanzibar Namba 12 ya mwaka 2003 pamoja na Sheria ya kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Namba 1 ya mwaka 2012 zimeundwa kwa lengo la kusimamia na kuimarisha utawala bora Nchini. Sambamba na hilo,

Serikali imetayarisha muongozo wa Haki za Binaadamu kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kwa lengo la kukuza uelewa wa wananchi juu ya masuala ya Haki za Binaadamu.

### 6.10 Kupunguza Umasikini

Juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuimarisha uchumi zimepelekea kupunguza umasikini wa chakula kutoka asilimia 13.18 mwaka 2005 mpaka asilimia 13.04 mwaka 2010 na umasikini wa mahitaji muhimu pia umepungua kutoka asilimia 49.07 mwaka 2005 mpaka asilimia 44.41 mwaka 2010. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya kwa Zanzibar uliofanyika mwaka 2009/2010 unaonesha kuwa kati ya mwaka 2004 na 2010, umaskini umepungua kwa kiasi kinachotia moyo taifa. Kiwango cha jumla cha umaskini kilipungua kwa asilimia 5 kutoka asilimia 49 mwaka 2004/05 hadi asilimia 44 mwaka 2009/10.

Kiwango cha kupungua kwa umaskini ni kikubwa zaidi katika maeneo ya mjini ikilinganishwa na maeneo ya vijijini. Katika maeneo ya mjini Umaskini ulipungua kutoka asilimia 40.54 mwaka 2004/05 hadi asilimia 35.97 mwaka 2010 wakati ambapo umaskini katika maeneo ya vijijini ulipungua kutoka asilimia 54.61 mwaka 2004/05 hadi asilimia 50.74 mwaka 2010. Kwa ujumla, kiwango cha umaskini kimekuwa kikipunguwa kwa asilimia moja kila mwaka katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010.

### 6.11 Udhibiti na Ukaguzi wa Hesabu za Serikali

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali ni pamoja na; kuimarika kwa kazi za Ukaguzi, kutoa ripoti za ukaguzi zilizokuwa na viwango vinavyokubalika Kimataifa na kwa wakati muafaka pamoja na kuongezeka kwa viwango vya taaluma ya ukaguzi kwa Watendaji wa Ofisi. Aidha, Ofisi imejenga majengo ya kisasa ya Ofisi Unguja na Pemba ambayo yanawezesha utoaji wa huduma kuwa katika mazingira bora.



*Rais wa Awamu ya Saba wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, akikata utepe kuashiria ufunguzi wa Jengo jipya la Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali liliopo Maisara Zanzibar Septemba 13, 2012.*

# SURA YA SABA

## CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA

### 7.1 Utangulizi

Katika kipindi hiki cha miaka 50 tangu Mapinduzi Matukufu ya Mwaka 1964, ORMBLM imekuwa ikikabiliana na changamoto mbalimbali. Changamoto hizi zimekuwa chachu ya kuchukua hatua katika kufanikisha malengo yake. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

i. Uhaba wa watumishi wenye taaluma na uzoefu katika baadhi ya Idara na Taasisi mbalimbali za ORMBLM hasa katika Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi (Diaspora).

ii. Kukua kwa Ofisi za kufanyia kazi, kutanuka kwa teknolojia, kuongezeka kwa idadi ya wafanyakazi pamoja na mahitaji ya kiutendaji, hii inapelekea ORMBLM kwa sasa inakabiliwa na uhaba mkubwa wa sehemu za kufanyia kazi.

iii. Pamoja na mwamko mkubwa wa baadhi ya Idara na Taasisi za ORMBLM wa kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa kujenga Ofisi, bado Taasisi nyingi zinakabiliwa na changamoto ya uhaba na uchakavu wa majengo ya Ofisi. Taasisi ambazo zinazokabiliwa na changamoto hii ni pamoja na; Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi (Diaspora), Idara ya Mawasiliano Ikulu, Ofisi ya Ofisa Mdhamini wa ORMBLM Pemba na Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

iv. Baadhi ya Sheria zinazoongoza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zimepitwa na wakati.

v. Kutoeleweka vizuri kwa mipaka ya demokrasia katika Utawala Bora.

vi. Kasi kubwa ya ukuaji wa maendeleo ya teknolojia.

vii. Upungufu wa vitendea kazi vikiwemo kompyuta na vifaa vyake, samani na vifaa vya uchunguzi.

viii. Kutokuwa na takwimu sahihi za Diaspora na maeneo wanayoishi kwa wingi pamoja na shughuli wanazozifanya.

ix. Mabadiliko ya mara kwa mara ya miongozo ya kazi za ukaguzi duniani pamoja na mabadiliko ya kasi ya sayansi na teknolojia duniani ambapo Ofisi inalazimika kwenda sambamba na mabadiliko hayo ili kuongeza ufanisi.

x. Ufahamu mbaya wa wananchi kuhusu matokeo ya takwimu zinazotolewa za utekelezaji wa Mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini Zanzibar.

# SURA YA NANE

## MATARAJIO YA ORMBLM PAMOJA NA TAASISI ZAKE KATIKA MIAKA 50 IJAYO

### 8.1 Utangulizi

Katika kipindi cha miaka 50 ijayo ORMBLM pamoja na Taasisi zake ina matarajio yafuatayo:-

i. Kuimarika kwa taswira ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambapo wananchi watajenga imani kubwa zaidi kwa Rais wao.
ii. Kuimarika kwa Sera, Sheria na miongozo ya Serikali.
iii. Kuimarika kwa mipango ya Serikali inayozingatia matokeo ya tafiti.
iv. Kuongezeka kwa ushiriki, huduma na uwekezaji wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za nje.
v. Kuongezeka na kutumika ipasavyo fursa zinazopatikana kutokana na ziara zinazofanywa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar
vi. Ushiriki wa Zanzibar wenye tija katika kukuza mahusiano ya Kikanda na Kimataifa.
vii. Kuongeza matumizi ya teknolojia ya habari katika kurahisisha utoaji wa huduma ndani ya Taasisi za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
viii. Kujenga Ofisi ya kisasa itakayokidhi haja na kuwawezesha wafanyakazi wake kufanya shughuli zao kwa ufanisi na ubora wa hali ya juu.
ix. Kuimarisha majengo ya Ikulu na nyumba za Serikali zilizopo Unguja, Pemba, Dar es Salaam na Dodoma. Aidha, kujenga nyumba za wafanyakazi na walinzi sambamba na kufanya matengenezo ya nyumba hizo.
x. Kuwa na watumishi wa Serikali walio waaminifu na waadilifu kwa Ofisi wanazofanyia kazi na Serikali yao kwa ujumla. Aidha, kuhakikisha kuwa watumishi hao wanafanyakazi katika mazingira yaliyo salama.
xi. Kuimarika kwa chombo makini chenye tija na ufanisi kisichovumilia uwepo wa Rushwa na Uhujumu Uchumi ambacho kitaweza kubaini, kuzuia na kutokomeza vitendo vya rushwa na Uhujumu Uchumi.
xii. Kuimarika huduma za Utawala Bora na Haki za Binaadamu Zanzíbar.

xiii. Utekelezaji Mikakati ya Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini utahakikisha mipango ya Nchi inalenga katika kukuza uchumi na kuondoa umasikini wa kipato.

xiv. Kuwa na rasilimali watu wenye uwezo wa kumudu vyema utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

xv. Kuwa na vitendea kazi vya kutosha na vya kisasa ambavyo vitasaidia kuleta ufanisi wa haraka katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
S.L.P 2422
Website: www.ikuluzanzibar.go.tz
Zanzibar
Agosti, 2013